HABARI KITAIFA / MATANGAZO

TANZIA

Wanafamilia watatu wafariki dunia moto ukiteketeza nyumba

Na Robinson Wangiso,
MUSOMA

MSIBA umeikumba Manispaa ya Musoma baada ya watu watatu wa familia moja, akiwamo mtumishi wa Wizara ya Maji, kufariki dunia katika tukio la kusikitisha la nyumba yao kuteketea kwa moto.

Waliopoteza maisha katika mkasa huo ni Rochi Mkolekuwa (39), aliyekuwa Meneja wa Ubora wa Maji katika Maabara ya Mkoa wa Mara, mkewe Mariam Msigwa (34) pamoja na mtoto wao Rochi Shaban (4).

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana katika Mtaa wa Nyarusrya, Kata ya Rwamlimi, Manispaa ya Musoma, Mkoa wa Mara, wakati familia hiyo ikisadikiwa kuwa imelala usingizi mzito.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mara, Agostino Magere, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema chanzo cha moto huo hakijajulikana, huku uchunguzi wa kina ukiendelea.

Magere alisema walipokea taarifa za tukio hilo majira ya saa 10 usiku, lakini walipowasili eneo la tukio walikuta nyumba hiyo ikiwa tayari imeteketea kabisa, huku miili ya waathirika ikiwa bado ndani.

"Tulipofika tulikuta tayari nyumba imeshateketea na watu wote waliokuwa ndani walikuwa wamefariki dunia. Mwili wa baba ulikutwa sebuleni, huku miili ya mama na mtoto ikikutwa chumbani. Uchunguzi umeanza kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama," alisema Magere.

Aliongeza kuwa hadi sasa chanzo halisi cha moto huo hakijabainika na uchunguzi unaendelea kwa ushirikiano wa Jeshi la Polisi, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na mamlaka nyingine husika mkoani humo.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Manispaa ya Musoma wakati taratibu nyingine za kisheria zikiendelea.

Mashuhuda wa tukio hilo, akiwamo jirani wa familia hiyo Rhobi Chacha, walisema wananchi walistuka majira ya saa tisa usiku baada ya kuona moshi na moto mkali ukitoka katika nyumba hiyo.

"Wananchi walijaribu kusaidia, lakini haikuwezekana kuingia ndani kwa sababu geti lilikuwa limefungwa. Tulijaribu kulivunja kwa nguvu ndogo tulizokuwa nazo, lakini hatukufanikiwa," alisema Chacha.

Jirani mwingine, Bartazal Manyerere, alisema juhudi zote za uokoaji zilishindikana kutokana na moto kuwa mkali na vifaa hafifu vilivyokuwapo, huku familia hiyo ikiwa bado ndani ya nyumba hadi Jeshi la Zimamoto lilipofika na kukuta tayari wamepoteza maisha.



Mkuu wa wilaya ya Muheza, Ayub Sebabili, akizungumza na wananchi wa kata ya Magila wilayani Muheza, hivi karibuni katika mkutano wa hadhara kusikiliza kero zao. **PICHA: STEVE WILLIAM**

KILIMO

Ujenzi mfereji waleta neema kwa wakulima na wafugaji Meru

Na Mwandishi Wetu

ZAIDI ya wakulima na wafugaji 7,000 katika vijiji vya Ngabobo, Tank na Oltepes, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, wamepata nafuu kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa mfereji wa maji unaotumika kwa umwagiliaji mashambani na unyweshaji mifugo.

Mfereji huo wenye urefu wa kilometa 8.2 umeleta mabadiliko makubwa katika upatikanaji maji, hususan kipindi cha kiangazi ambacho mvua huwa haba.

Kupitia mradi huo, changamoto ya uhaba wa maji iliyokuwa ikikabili wakulima na wafugaji kwa miaka mingi imepungua kwa kiwango kikubwa na hivyo kuongeza tija katika shughuli za uzalishaji.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Zainabu Mwakwinya, alisema halmashauri kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imetekeleza miradi kadhaa ya maji iliyosaidia kutatua migogoro ya matumizi ya rasilimali hiyo muhimu.

"Kwa sasa katika halmashauri yetu hakuna tena matatizo makubwa ya maji katika maeneo mengi. Wakulima na wafugaji wanaendesha shughuli zao kwa pamoja bila migogoro kama ilivyokuwa awali," alisema Mwakwinya.

Diwani wa Ngabobo, Gabriel Kinoa, alisema kabla ya ujenzi wa mfereji huo kulikuwapo mfereji wa asili uliokuwa na upotevu mkubwa wa maji na kusababisha maji kuchelewa kuwafikia wananchi mashambani.

"Changamoto ya maji ilikuwa kubwa sana, hasa kipindi cha kiangazi. Hata hivyo, mfereji huu mpya umepunguza kwa kiasi kikubwa muda wa maji kufika mashambani.

"Zamani ilichukua zaidi ya saa moja, lakini sasa ni chini ya saa moja tu baada ya kufunguliwa maji huwafikia wakulima," alisema Kinoa.

Manufaa ya mfereji huo yameonekana pia katika ongezeko la uzalishaji mazao. Mkulima wa nyanya na ulezi katika kijiji cha Ngabobo, Benjamin Mollel, alisema kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji na kuboresha kipato cha wakulima.

"Hivi sasa, kipindi cha mavuno, malori kati ya 10 hadi 12 yanaingia mashambani kuchukua mazao, hasa nyanya.

"Zamani tulikuwa tunamwagilia takribani hekta 400 tu, lakini sasa tumefikia zaidi ya hekta 1,300. Tunashukuru sana serikali na TASAF kwa ujenzi wa mfereji huu," alisema Mollel.

Mkulima na mkazi wa kijiji cha Oltepes, Josephine Naiso, aliwataka wananchi kuutunza mfereji huo ili uendelee kuwanufaisha kwa muda mrefu.

"Zamani familia zilikuwa hazitulii kwa sababu ya kutafuta maji. Wanaume wetu walikuwa wakishinda kwenye kazi za kijiji kusafisha mifereji ya asili.

"Sasa hali imebadilika. Kaya zinapata kipato zaidi, zinajenga nyumba za kisasa na maisha yameimarika. Tunashukuru sana kwa mradi huu," alisema Naiso.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Meru, Edwin Serunkuma, alisema mradi huo uliibuliwa na wananchi wenyewe Januari 2025, ambapo zaidi ya Sh. milioni 460 zilitumika kujenga mfereji wa kilometa 8.2.

"Aprili 2025 tulipokea fedha za awali na Mei tukaanza ujenzi. Tulianza na kilometa moja iliyogharimu Sh. milioni 66, kisha tukakamilisha kilometa 7.2 kwa gharama ya Sh. milioni 401," alisema Serunkuma.

Aliongeza kuwa maji kutoka mfereji huo yanahudumia vijiji vya Wilaya ya Meru pamoja na Wilaya ya Longido, ambako wananchi wameweka utaratibu wa zamu za matumizi ili kuhakikisha rasilimali hiyo inawanufaisha wote kwa usawa.

KUPOTEA KWA CHETI



EDWARD THOMAS GERVAS, Anatangaza kupotea kwa Cheti Cha Darasa la SABA chenye Index No.PS **1301061/021** kilichotolewa na Baraza la Mtihani kupitia **NUNDU PRIMARY SCHOOL** Mwaka 2019.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi. **PHQ/TAB/TAB/34/2026**

KUPOTEA KWA CHETI



JAPHET JOVENT ERNEST anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Nne chenye Index Number **S3627/0045** kilichotolewa na Baraza la Mitihani Kupitia **MAGNUS SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2019.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi. **PHQ/DAR/ILA/184786/2025.**

IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE
PROBATE AND ADMINISTRARION CAUSE NO.31651

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE WILLIAM MASAWE KITOMARY

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION

BY SALOME ANDREA MAYANGE

GENERAL CITATION
(Rule 75 of probate Rules GN 369 Of 1963)

All Persons claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **19th day January 2026**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

KUPOTEA KWA CHETI



SHUMINA MAAGI CEPTINE, anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Nne chenye index number **S.1119-0083** kilichotolewa na Baraza la Mitihani Kupitia **BIASHARA SECONDARY SCHOOL MOMBASA UNGUJA ZANZIBAR** Mwaka 2023.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi. **MAD/RB/4537/2025.**

KUPOTEA KWA VYETI



STELLA HAKIKA KAJANGE, Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S0341/0096/2018** kilichotolewa na **SANGU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Cheti cha kidato cha SITA chenye index namba **S.0341/0629** kilichotolewa na SANGU Secondary School mwaka 2021. Cheti cha kidato cha **DIPLOMA IN CLINICAL MEDICINE** chenye **NS.0341/0096/2018** kilichotolewa na **EXCELLENT COLLEGE OF HEARTH ALLIED SCIENCE** Mwaka 2024. Certificate of Enrollment Chenye Reg No.MCT ER26180 .Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya **PHQ/DAR/UBU/1895/2026**